

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI**

---

**MAONI YA KAMATI KUHUSU MUSWADA WA MAREKEBISHO YA SHERIA  
MBALIMBALI ZA FEDHA NAMBA 13 WA MWAKA 2022**

Ofisi ya Bunge,  
S.L.P 941,  
**DODOMA.**

22 Septemba, 2022

## YALIMYOMO

<b>1.0</b>	<b>UTANGULIZI .....</b>	<b>2</b>
<b>1.1.</b>	<b>Uchambuzi wa Muswada .....</b>	
3		
<b>2.0.</b>	<b>MADHUMUNI YA MUSWADA .....</b>	<b>3</b>
<b>3.0.</b>	<b>MAONI NA USHAURI WA KAMATI KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA MABADILIKO YA SHERIA MBALIMBALI NA 6 WA MWAKA 2021. ....</b>	<b>4</b>
<b>3.1.</b>	<b>Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura ya 147 (The Exice Management and Tarrif) Act, Ca147) .....</b>	<b>4</b>
<b>3.2.</b>	<b>Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura 332 (<i>The Income Tax Act, (Cap 332)</i>) .....</b>	
5	<b>3.3. Sheria ya Madini Sura, Sura 123 (The Mining Act, (Cap 123) .....</b>	
5	<b>3.4. Sheria ya Ushuru wa Mafuta ya Barabara ( The road Fuel Toll Act, (Cap 220) ...</b>	
6	<b>3.5. Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura ya 148 (Value Added Act, (Cap 148) .....</b>	
		<b>7</b>
<b>4.0.</b>	<b>MAONI NA MAPENDEKEZO YA JUMLA .....</b>	<b>7</b>
<b>4.1.</b>	<b>Kufanya tathmini na Utafiti ya Faida na Hasara ya Misamaha ya Kodi ambayo inatolewa na Serikali. ....</b>	<b>7</b>
<b>4.2.</b>	<b>Misamaha ya Kodi kwa Pato la Taifa (Tax exemption/GDP) .....</b>	
8	<b>4.3. Serikali kuimarisha Vitengo vya utafiti wa Sera za Mapato ili kuiwezesha Serikali kuwa na Taarifa za uhakika pindi inapoandaa sera za mapato. ....</b>	<b>8</b>
<b>5.0.</b>	<b>HITIMISHO .....</b>	<b>8</b>

# **MAONI YA KAMATI KUHUSU MUSWADA WA MAREKEBISHO YA SHERIA**

## **MBALIMBALI ZA FEDHA NAMBA 13 WA MWAKA 2022**

### **1.0 UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (1) (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020 naomba kutoa maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali za Fedha Namba 13 wa Mwaka 2022 **The Written Laws (Financial Provisions) (Ammendment) Act, 2022**

**Mheshimiwa Spika**, tarehe 19 Septemba, 2022, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango aliwasilisha Bungeni Mapendekezo ya Serikali kuhusu Muswada wa Mabadiliko ya Sheria za Fedha na 13 na baada ya kuwasilisha Muswada huo, Mheshimiwa Spika uliiagiza Kamati ya Kudumu ya Bajeti kuuchambua muswada huo ili baadaye maoni yake yawasilishwe Bungeni.

#### **1.1. Uchambuzi wa Muswada**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imefanya uchambuzi wa muswada huu kwa kupitia kifungu kwa kifungu kwa madhumuni ya kujielimisha maudhui ya kila kifungu na kupendekeza marekebisho katika maeneo ambayo yanahitaji maboresho. Baada ya kujiridhisha na maudhui ya Muswada, tarehe 19 hadi 21 Septemba, 2022 Kamati ilifanya majadiliano ya kina na Waziri wa Fedha na Mipango, Waziri wa Kilimo; Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, pamoja na Watendaji wa Wizara. Aidha, Kamati pia ilikutana na wadau kwa ajili ya kupokea mapendekezo na maoni yao juu ya marekebisho yanayopendekezwa. Wadau waliofika kwenye Kamati ni Aliko Vintage.

### **2.0. MADHUMUNI YA MUSWADA**

**Mheshimiwa Spika**, Muswada huu una madhumuni makubwa matatu kama ifuatavyo:-

- i. Kuchochea uzalishaji wa mbolea nchini ili zipatikane kwa bei nafuu; ii. Kutoa vivutio maalumu kwa miradi ya kimkakati na mahiri ili kuchochea uwekezaji kwenye miradi mikubwa yenyе kuleta mapinduzi ya kiuchumi; na

- iii. Kuchochaea uzalishaji ndani hasa wa bidhaa za magunia na mvinyo ili kuchochaea kilimo cha mazao ya zabibu na katani.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kutazama madhumuni haya ya muswada nitoe pongezi kwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hasan Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuonyesha nia ya dhati ya kuvutia wawekezaji na kutekeleza miradi mikubwa inayoleta mapinduzi ya kiuchumi. Kamati inaamini kwa masharti yaliyoko kwenye muswada huu Mhe Rais atakuwa ameonyesha kwa vitendo namna bora ya kutanzua vikwazo vinavyokwamisha utekelezaji wa miradi ya kimkakati.

### **3.0. MAONI YA KAMATI KUHUSU MUSWADA WA MAREKEBISHO YA SHERIA MBALIMBALI ZA FEDHA NAMBA 13 WA MWAKA 2022.**

**Mheshimiwa Spika**, Muswada huu unafanya mabadiliko katika sheria tano za Kodi ambazo ni Sheria ya Ushuru wa Bidhaa Sura ya 147, Sheria ya Kodi ya Mapato Sura 332, Sheria ya Madini Sura ya 123, Sheria ya Ushuru wa Mafuta 220 na Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) Sura ya 148. Baada ya majadiliano ya kina baina ya Kamati na Serikali, Kamati ina maoni na mapendekezo yafuatayo: -

#### **3.1. Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura ya 147 (The Excise Management and Tarrif) Act, Ca147)**

**Mheshimiwa Spika**, Serikali inapendekeza kurekebisha kifungu cha 128 ili kumpa Mamlaka Waziri mwenye dhamana na masuala ya fedha, baada ya kupata idhini ya Baraza la Mawaziri kusamehe ushuru kwenye bidhaa zitakazotumika katika utekelezaji wa miradi ya uwekezaji mahiri na ya kimkakati itakayoidhinishwa na Kamati ya Taifa ya Uwekezaji (NISC) pamoja na kupandisha ushuru wa Bidhaa za mvinyo kutoka nje kutoka **shilingi 2,466.45** hadi **shilingi 5,600** kwa lita ili kulinda wakulima wa ndani wa zao la zabibu.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilibaini kuwa nchi za jirani zinatoza kati ya **shilingi 5,000** hadi **5,500** kwa lita ya mvinyo unaotoka nje, hivyo hatua hii inahuisha viwango vinavyotozwa katika nchi wanachama wa Afrika Mashariki. Aidha, hatua hii inaleta usawa wa kiushindani kati ya wazalishaji wa zao la zabibu nchini dhidi

ya mataifa mengine ambayo yameendelea sana katika uzalishaji wa zao hili. Hivyo, Kamati inakubaliana na pendekozo hili ambalo lina nia njema la kusaidia na kuinua viwanda vya ndani na kuwa shindani. Hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha inasimamia ubora wa mvinyo unaozalishwa ndani ya nchi pamoja na kuchochea kilimo cha aina mbalimbali za zabibu ili kuhakikisha kwamba malighafi hii muhimu kwa utengenezaji wa mvinyo inapatikana ndani ya nchi. Aidha, Kamati ilishauri Serikali na Serikali ilikubali kuweka sharti kwamba, endapo msamaha utatumika kwa namna ambayo hajakusudiwa, msamaha huo utaondolewa na muhusika atalazimika kulipa ushuru stahiki. Marekebisho hayo yanaonekana kupitia jedwali la marekebisho la Serikali.

### **3.2. Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura 332 (*The Income Tax Act, (Cap 332)*)**

**Mheshimiwa Spika**, Kifungu cha 10 kinarekebishwa ili kujumuisha uwekezaji mahiri uliodhinishwa na Kamati ya Taifa ya Uwekezaji- NISC, katika wigo wa maeneo ambayo Waziri mwenye dhamana ya Masuala ya fedha anaweza kutoa msamaha wa kodi ya mapato. Aidha, mapendekezo haya yanabainisha kwamba misamaha ya kodi ya mapato itakayokuwa inatolewa kupitia mikataba ambayo Serikali inaingia na wawekezaji ndio itatumika wakati wa kukokotoa Kodi ya Mapato.

**Mheshimiwa Spika**, hatua hii ina nia njema ya kutanzua mkwamo wa Miradi ya Kimkakati ya wawekezaji mahiri. Uzoefu unaonyesha kuwa kuna baadhi ya wawekezaji mahiri wametumia mikataba yao vibaya kuhakikisha kwamba Serikali haipati mapato yake inayostahili. Aidha, Kamati ilishauri Serikali na Serikali ilikubali kuweka sharti la kwamba endapo msamaha utatumika kwa namna ambayo hajakusudiwa, msamaha huo utaondolewa. Marekebisho hayo yanaonekana kupitia jedwali la marekebisho la Serikali.

### **3.3. Sheria ya Madini Sura, Sura 123 (*The Mining Act, (Cap 123)*)**

**Mheshimiwa Spika**, Kifungu cha 87 (1) kinarekebishwa ili kupunguza kiwango cha mrabaha kwa malighafi za mbolea zinazochimbwa hapa nchini, kutoka **asilimia 3** hadi **asilimia 1**. Kamati imekubaliana na mapendekezo ya Serikali. Hata hivyo, imeishauri Serikali hatua hii iwe ni ya mwaka mmoja ili kuangalia endapo inatimiza malengo yaliyokusudiwa. Aidha, kwa kuwa sekta ya mbolea imepata msamaha

kwenye kodi ya ongezeko la thamani kwa kutozwa kwa asilimia sifuri na pili kupunguziwa mrabaha ni vyema sasa Serikali ikaweka utaratibu wa kupanga bei elekezi kwa mbolea inayozalishwa ndani ili kuhakikisha mbolea inamfikia mkulima kwa bei nafuu. Endapo suala la bei litaachiwa kwa wamiliki wa viwanda ni wazi kwamba manufaa haya hayatamfikia mkulima na badala yake wazalishaji watajitengenezea faida ya kupindukia (super normal profit).

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilishauri Serikali na ikakubali kuongeza madini ya chokaa yanayotumika kwa ajili ya kuzalisha mbolea nayo kutozwa mrabaha kwa **asilimia 1** ili pia viwanda vinavyotumia madini hayo navyo kunufaika na punguzo hilo. Lengo la msingi ikiwa ni kuongeza uzalishaji wa mbolea ndani ya nchi na kupunguza bei kwa wakulima.

### **3.4. Sheria ya Ushuru wa Mafuta ya Barabara ( The road Fuel Toll Act, (Cap 220)**

**Mheshimiwa Spika**, kifungu cha 8 kinarekebishwa ili kumpa Waziri mamlaka ya kusamehe ushuru wa mafuta kwa miradi ya uwekezaji mahiri na mahiri maalum itakayoidhinishwa na Kamati ya NISC. Uzoefu unaonyesha kwamba kama kuna moja ya msamaha ambao umetumika vibaya ni msamaha wa ushuru wa mafuta. Hivyo, kutokana na uzoefu huo Kamati inaishauri Serikali masuala yafuatayo:-

- i. Kuwepo na muda maalumu wa kusamehe ushuru kwenye mafuta baada ya mradi kukamilika;
- ii. Kwa kuwa mfumo wa kuagiza mafuta ni wa pamoja lazima kuwe na namna ama ya kutofautisha kwa vinasaba au uuza ji wake ili kuondoa mwanya wa matumizi mabaya;
- iii. Kuweka mfumo wa usimamizi ili kuzuia mafuta yaliyokuwa yatumike kwa ajili ya miradi kutumika katika shughuli tofauti;
- iv. Inashauriwa pia kwamba sharti la kuondoa msamaha liliopo katika kanuni za Sheria hii litekelezwe endapo itaonekana msamaha umetumika vibaya.

**Mheshimiwa Spika**, Ushauri huu wa kamati ni kuhakikisha kwamba msamaha huu usije ukasababisha uuza ji holela wa mafuta nchini (dumping). Aidha, kamati ilishauri Serikali na Serikali ilikubali kuweka sharti la kwamba endapo msamaha

utatumika kwa namna ambayo hajjakusudiwa, msamaha huo utaondolewa na muhusika atalazimika kulipa ushuru stahiki. Marekebisho hayo yanaonekana kupitia jedwali la marekebisho la Serikali.

### **3.5. Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura ya 148 (*Value Added Act, Cap 148*)**

**Mheshimiwa Spika**, Kifungu cha 6 kinafanyiwa marekebisho ili kujumuisha uwekezaji mahiri ulioidhinishwa na Kamati ya NISC, ambapo Waziri mwenye dhamana ya masuala ya fedha anaweza kutoa msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani. Aidha, kuongeza kifungu kipyga cha 55A kwa kutoza kodi ya ongezeko la thamani kwa kiwango cha 0 kwa mbolea inayozalishwa ndani ya nchi ili kuleta unafuu kwa wakulima na watumiaji wa mbolea. Vilevile, kurekebisha jedwali ili kusamehe kodi ya ongezeko la thamani kwa magunia ya mkonge yanayotengenezwa nchini inayotambulika kwa HS Code 6305.90.00 na malighafi inayotambulika chini ya HS Code 7229.90.00 ambayo hutumika kutengeneza mitungi ya gesi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inakubaliana na Serikali kwa mabadiliko katika sheria hii kwa lengo la kupunguza bei ya magunia yanayozalishwa ndani. Hata hivyo, ilishauri Serikali na ikakubali kuweka ukomo wa mwaka mmoja ili kuangalia endapo msamaha huo unaleta manufaa yaliyokusudiwa. Aidha, Kamati ilishauri kwamba kuhusu msamaha wa malighafi za kuzalisha mitungi ya gesi usitolewe katika kipindi hiki kwa sababu unaathiri mapato ya Serikali. Serikali ilikubali pendekezo hilo la Kamati na ibara ya 15 (b) ya muswada iliondolewa kama inavyoonekana kwenye jedwali la marekebisho la Serikali.

## **4.0. MAONI NA MAPENDEKEZO YA JUMLA**

**Mheshimiwa Spika**, masuala mengine yaliyojadiliwa katika Kamati wakati wa kuitisha Muswada wa Sheria ya Fedha ni kama ifuatavyo: -

### **4.1. Kufanya tathmini na Utafiti ya Faida na Hasara ya Misamaha ya Kodi ambayo inatolewa na Serikali.**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishuri Serikali kuhakikisha kuwa inajiridhisha na misamaha ya kodi pamoja vivutio vingine vinavyolenga kuvutia uwekezaji

nchini. Kujiridhisha kwa hatua hizo ili kuhakikisha kuwa inaleta matokeo tarajiwa na sio kuipotezea Serikali mapato. Aidha, kuwepo na usimamizi mzuri wa misamaha inayotolewa na Serikali kwa wawekezaji mahiri pamoja na wa Kimkakati.

#### **4.2. Misamaha ya Kodi kwa Pato la Taifa (Tax exemption/GDP)**

**Mheshimiwa Spika**, Misamaha ya Kodi ni hatua ya Sera za Mapato ambayo huwa na malengo mbalimbali kama vile kuchochea uzalishaji, kupunguza gharama za huduma au bidhaa, kugawanya rasilimali na kuchochea ukuaji wa sekta. Hata hivyo malengo tuliojiwekea katika Mpango wa Miaka mitano misamaha haitakiwi kuzidi asilimia 1 ya pato la Taifa. Hivyo ni wakati sasa kwa Serikali kufanya Tathmini ya kina ya misamaha yote ya kodi iliyotolewa na kuona endapo misamaha hiyo imefikia malengo yaliyokusudiwa.

#### **4.3. Serikali kuimarisha Vitengo vya utafiti wa Sera za Mapato ili kuiwezesha**

**Serikali kuwa na Taarifa za uhakika pindi inapoandaa sera za mapato.**

**Mheshimiwa Spika**, Kuna haja ya msingi ya kuimarisha vitengo vya utafiti wa Sera za Mapato na hasa kodi kwa kuvitengea rasilimali watu na fedha za kutosha ili vitekeleze majukumu yake kikamilifu. Kamati inaamini mabadiliko yanayofanywa mara kwa mara katika sheria za Kodi ni kutokana na kutokuwa na utafiti wa kina katika sera za mapato.

### **5.0. HITIMISHO**

**Mheshimiwa Spika**, naomba kutumia fursa hii kwanza kukushukuru wewe, Mheshimiwa Spika kwa kunipa fursa hii ili niweze kuwasilisha maoni ya Kamati kuhusu Muswada wa Mabadiliko ya Sheria za Fedha Na 13 wa Mwaka 2022 mbele ya Bunge lako Tukufu. Pili nimshukuru Mhe Mussa Azzan Zungu, Mb - Naibu Spika kwa ushirikiano wake. Aidha napenda nimshukuru Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb), Waziri wa Fedha na Mipango, Mhe. Hassan Chande, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mhe. Hussen Bashe Waziri wa Kilimo, Mhe. Exaud Kigahe Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara,

Ofisi ya Mwanasheria Mkoo wa Serikali na Ofisi ya Muandishi wa Sheria wa Bunge kwa ushirikiano wao kwa Kamati. Aidha, napenda kuwashukuru Watendaji wote wa Wizara ya Fedha na Mipango na Ofisi ya Mwanasheria Mkoo wa Serikali kwa maoni na ushauri wao ulioiwezesha Kamati kuchambua Muswada hadi kufikia hatua hii.

**Mheshimiwa Spika**, Napenda Kumshukuru Mhe. Omari Kigua Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti na vilevile napenda kuwashukuru Wajumbe wa kamati ya Bajeti kwa umakini, umahiri na uvumilivu wao katika kipindi chote cha uchambuzi wa Muswada huu, hasa ukizingatia kwamba muda haukuwa rafiki sana. Wajumbe hao ni:

1. Mhe. Sillo Daniel Baran, Mb	Mwenyekiti
2. Mhe. Omari Mohamed Kigua, Mb	M/Mwenyekiti
3. Mhe. Ali Hassan Omar King, Mb	Mjumbe
4. Mhe. Issa Jumanne Mtemvu, Mb	Mjumbe
5. Mhe. Oran Manase Njeza, Mb	Mjumbe
6. Mhe. Josephat Sinkamba Kandege, Mb	Mjumbe
7. Mhe. Leah Jeremiah Komanya, Mb	Mjumbe
8. Mhe. Joseph George Kakunda, Mb	Mjumbe
9. Mhe. Shally Josepha Raymond, Mb	Mjumbe
10. Mhe. Subira Khamis Mgusu, Mb	Mjumbe
11. Mhe. Esther Nicholas Matiko, Mb	Mjumbe
12. Mhe. Jonas William Mbunda, Mb	Mjumbe
13. Mhe. Mariam Madalu Nyoka, Mb	Mjumbe
14. Mhe. Juma Hamad Omar, Mb	Mjumbe
15. Mhe. Kwagilwa Reuben Nhamanilo, Mb	Mjumbe
16. Mhe. Tarimba Gulam Abbas, Mb	Mjumbe
17. Mhe. Amina Iddi Mabrouk, Mb	Mjumbe
18. Mhe. Riziki Said Lulida, Mb	Mjumbe
19. Mhe. Zaytun Seif Swai, Mb	Mjumbe
20. Mhe. Shamsi Vuai Nahodha, Mb	Mjumbe
21. Mhe. Dkt Charles Kimei, Mb	Mjumbe
22. Mhe. Mariam Kisangi, Mb	Mjumbe

**Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee naomba kumshukuru Katibu wa Bunge Bi. Nenelwa Mwihambi *ndc* pamoja na watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Aidha, napenda kuishukuru Sekretarieti ya Kamati ya Bajeti ikiongozwa na Ndg. Michael Kadebe, Mkurugenzi wa Idara ya Bajeti kwa kuratibu shughuli za Kamati pamoja na kutoa ushauri wa kitaalamu na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

Daniel Baran Sillo (Mb)

**MWENYEKITI KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI**

22 Septemba, 2022